Kifua Kikuu

# Je, kipi kitatokea ikiwa nilipata chanjo ya BCG?

Nchi nyingi nje ya Marekani hutumia chanjo ya bacilli BCG au bacilli Calmette-Guerin, kama sehemu ya mpango wake wa kudhibiti Kifua Kikuu, hasa kwa watoto wachanga. Ufanisi wa chanjo ya BCG hutofautiana na kinga dhidi ya ugonjwa wa Kifua Kikuu hupungua kwa kiasi kikubwa kwa kadiri muda unavyosonga.

BCG inaweza kusababisha mmenyuko chanya wa uongo wakati unapotumia vipimo vya ngozi vya Kifua Kikuu. Vipimo vya damu vya kifua kikuu haviathiriwi na chanjo ya BCG na havitoi matokeo ya uongo ya kipimo chanya. Ikiwa ulipokea BCG (kama chanjo au kama tiba ya saratani), kipimo cha damu kinapendekezwa.

## Mpango wa Kifua Kikuu wa Iowa HHS


Lucas State Office Building
321 East 12th Street
Des Moines, IA  50319-0075


**hhs.iowa.gov/public-health/tb**

**KWA MAELEZO ZAIDI KUHUSU KIFUA KIKUU, TEMBELEA**

- **https://www.cdc.gov/tb/**
- **https://www.lung.org**
- **https://www.thoracic.org**


IOWA Health and Human Services
Public Health

06 / 2024


Jifunze ukweli kuhusu

# Kifua Kikuu (TB)




IOWA Health and Human Services
Public Health

**Kifua Kikuu (TB)** si ugonjwa tu wa kale. Ulimwenguni kote, TB huua watu wengi zaidi ya ugonjwa wowote wa kuambukiza, ikijumuisha VVU. TB ambayo haikutibiwa huua mwathirika mmoja kati ya wawili.

### TB NI NINI?

TB ni ugonjwa unaosababishwa na bakteria (viini) ambavyo husambazwa kutoka kwa mtu mmoja hadi kwa mtu mwingine kwa njia ya hewa. TB kwa kawaida huathiri mapafu (TB ya mapafu) lakini inaweza pia kuathiri sehemu zingine za mwili, kama vile ubongo, vifundo vya limfu au uti wa mgongo.

### JE, TB HUSAMBAZWAJE?

Viini vya TB husambazwa pale mtu mwenye ugonjwa wa TB anapokohoa, kupiga chafya, kuzungumza au kuimba. Watu ambao huvuta hewa ile ndani yenye viini vya TB wanaweza kupata maambukizi. Si kila anayeambukizwa TB uugua. Kwa sababu hiyo, kuna hali mbili zinazohusiana na TB: maambukizi yaliyojificha ya TB (LTBI) na ugonjwa wa TB.

## Je, kuna tofauti gani kati ya LTBI na ugonjwa wa TB?

### LTBI

Watu wenye LTBI wana viini vya TB ndani ya miili yao lakini hawaugui kwa sababu viini hivyo havifanyi kazi. Watu ambao hawakutibiwa LTBI wako katika hatari ya kupata ugonjwa wa TB. Kutibiwa LTBI kunapendekezwa kwa kiasi kikubwa ili viini visianze kufanya kazi na kusababisha ugonjwa wa TB.

### UGONJWA WA TB

Watu wenye TB uugua kutokana na viini vya TB ambavyo vinafanya kazi katika miili yao. Dalili za ugonjwa wa TB ya mapafu ni: kukohoa kwa zaidi ya wiki tatu, kupungua uzito bila sababu, joto kali, kutoka jasho usiku na uchovu. Watu wenye ugonjwa wa TB wanaweza kusambaza viini vya TB kwa watu wengine. Ugonjwa wa TB unaponywa kwa kutumia matibabu yenye ufanisi. Wasipotibiwa, watu wenye ugonjwa wa TB wanaweza kuwa wagonjwa sana na kufa.

## Je, unapimaje TB?

### KIPIMO CHA NGOZI

Kipimo cha ngozi cha TB ndicho aina ya kipimo cha kawaida zaidi cha TB. Hufanyika kwa kuchoma sindano yenye kiasi kidogo cha kuowevu (tuberculin) chini ya ngozi ya mkono wako. Mtoa huduma wako wa afya atakuchunguza mkono wako saa 48-72 baada ya kipimo cha TB ili kubaini ikiwa matokeo ya kipimo ni “chanya” au “hasi.”

### VIPIMO VYA DAMU

Njia nyingine ya kupima TB ni kwa kutumia kipimo maalum cha damu. Kipimo cha damu hupima jinsi mfumo wako wa kingamaradhi unavyoshughulika na viini ambavyo husababisha TB. Mtoa huduma wako wa afya atatoa damu kutoka kwenye mkono wako ili kufanya kipimo hiki. Ni ziara moja inayohitajika na kwa kawaida matokeo hupatikana ndani ya siku chache.

| LTBI | Ugonjwa wa TB (wa mapafu) |
|---|---|
| Kipimo chanya cha TB (kipimo cha damu au ngozi) | Kipimo cha TB (ngozi au damu) kwa kawaida huwa chanya lakini kinaweza kuwa hasi au kisichobainika |
| Eksirei ya kifua ya kawaida | Eksirei ya kifua isiyo ya kawaida |
| Hakuna dalili | Dalili: kukohoa kwa zaidi ya wiki 3, kupungua uzito bila sababu, kutoka jasho usiku na uchovu |
| Isiyo ya kuambukizanwa | Ya kuambukizanwa |
| Kutibiwa LTBI kunapendekezwa | Huponywa kwa kutumia dawa za kuzuia bakteria |



### ITAKUWAJE IKIWA HICHO KIPIMO CHA TB NI CHANYA?

Ikiwa kipimo cha ngozi au damu ni chanya, kuna uwezekano kuwa una maambukizi ya viini vya TB. Mtoa huduma wako wa afya ataagiza ufanyiwe eksirei ya kifua ili kuwa na uhakika kama maambukizi ya TB hayajafikia kuwa ugonjwa wa TB. Ikiwa unakohoa, au ikiwa eksirei si ya kawaida, vipimo vya ziada vinaweza kuwa na umuhimu.

### IKIWA KIPIMO CHANGU CHA TB NI CHANYA, JE! NITUMIE DAWA?

Ndio, matibabu mara zote hupendekezwa kwa watu ambao kipimo chao cha TB ni chanya. Kanuni za kutibu LTBI zinazopendekezwa kwa kawaida zinahusisha kutumia dawa za kuzuia bakteria kwa miezi 3-4. Kwa kutumia dawa za kuzuia bakteria ili kutibu LTBI, unaweza kupunguza hatari yako ya kupata ugonjwa wa TB kwa zaidi ya 70-90% maishani mwako. Ni muhimu sana kutumia dawa hizo zote za kuzuia bakteria ili kuzuia kuendelea kwa LTBI hadi kuwa ugonjwa wa TB.

Ugonjwa wa TB unaweza kutibiwa kwa kutumia dawa kadhaa za kuzuia bakteria kwa miezi 6-12. Ni muhimu sana kwamba watu wenye ugonjwa wa TB wamalize dawa zao za kuzuia bakteria na wazitumie kama ilivyoagizwa. Ikiwa watu wataacha kutumia dawa za kuzuia bakteria mapema sana, wanaweza kuugua tena. Ikiwa hawatatumia dawa za kuua bakteria kama inavyotakiwa, viini ambavyo bado viko hai vinaweza kuwa na uwezo wa kukinzana na dawa za kuua bakteria. Mpango wa Kudhibiti TB wa Iowa HHS, hutoa dawa za TB kwa ajili ya kutibu LTBI na ugonjwa wa TB bila malipo.